

SHUGHULI ZA KISWAHILI

GRADE 4 - 2020

Jina

Jinsia: Mvulana

Msichana

Jina la shule

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Swali la 1	Swali la 2	Swali la 3	Swali la 4
Idadi ya alama	10	20	5	15
Alama sahihi				

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali (alama 10)

Musa alifanya ziāra ya kumzuru babu yake. Alifika kijijini wakati wa jioni.

Babu alimkaribisha Musa kwa furaha tele. Babu alilifungua kufuli lililokuwa kwenye tumbuu. Wote wakaingia sebuleni. Aliuweka mzigo wake kwenye mtoto wa meza. Kwa kuwa mwangaza ulikuwa hafifu, babu alibofya swichi na balbu ikasambaza mwangaza kote chumbani.

Nyanya alimwandalia mjukuu wake chajio mezani. Kwa kuwa baridi ilikuwa imeanza kuingia, babu alimpa koti refu akalivaa. Koti hilo lilikuwa limemfika kwenye goti. Baada ya kufanya maombi na kumsimulia hadithi, Musa alielekezwa kwenye chumba chake cha kulala. Nyanya alifunga neti kwenye fremu iliyokuwa darini kisha akaifunga kwenye tendegu la kitanda. Musa aliingia kitandani na kulala fofof!

1. Musa alifika kwa babu yake wakati gani? (Alama 1)

2. Kabla ya Musa na babu kuingia sebuleni ni kitu gani kilifanyika? (Alama 1)

3. Taja vitu vilivyokuwa kwenye sebule ya babu (Alama 4)

(a) _____

(b) _____

(c) _____

(d) _____

4. Kwa nini babu alibofya swichi? (Alama 1)

5. Dari ni _____ (Alama 1)

6. Kabla ya kulala Musa alifanyiwa nini? (Alama 2)

2. **LUGHA (Alama 20)**

1. **Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo (alama 2)**

(a) Pika _____

(b) Nyunyuzia _____

2. **Chagua kivumishi, nomino na kitenzi katika sentensi:**

Mwalimu mrefu alisimama darasani. (Alama 3)

3. Maneno yanayotoa maelezo jinsi kitendo kinavyofanyika huitwaje? (Alama 1)

4. Tambua kiwakilishi katika sentensi:

Kabati lililonunuliwa ni zuri (**Alama 1**)

5. Chagua jawàbu sahihi (Alama 3**)**

(a) Cherehani _____ (nzuri, mzuri, kizuri) ni chetu.

(b) Chagua kielezi:

Yaya alipika polepole _____

(c) Tunga sentensi ukitumia nomino ifuatayo:

Televisheni _____

6. Chagua jawabu lilio sahihi

1. Tegua vitendawili:

(a) Pitia huku nami nипитие kule tupatane pale _____ (**Alama 1**)

(b) Huko ng'o na kule ng'o _____ (**Alama 1**)

2. Jibu la salamu 'shikamoo' ni _____ (**Alama 1**)

3. Unda vitanzandimi ukitumia silabi za sauti zifuatazo: (**Alama 4**)

(a) p/b _____

(b) t/d _____

(c) k/g _____

(d) ch/j _____

4. Tunga sentensi moja sahihi ukitumia maneno: (**Alama 3**)

papa/baba _____

5. Chora meza na uonyeshe mvungu wake. (Alama 5)

(1) Alama 1

(2) Alama 4

(3) Alama 5

(4) Alama 6

(5) Alama 7

4. KUANDIKA (Alama 15)

Andika sentensi tano kuhusu 'Mwalimu wako wa darasa'.

(1) Alama 1

(2) Alama 2

(3) Alama 3

(4) Alama 4

(5) Alama 5

(6) Alama 6

(7) Alama 7

(8) Alama 8

(9) Alama 9

(10) Alama 10

(11) Alama 11

(12) Alama 12

(13) Alama 13

(14) Alama 14

(15) Alama 15